# TAARIFA KWA UMMA

Dodoma, 03/06/2024

Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania imetakiwa kuangalia upya sheria za usafiri ardhini kwa kuzifanyia mapitio na utafiti wa kina kwa kuwa zimeonekana kutodhibiti kikamilifu ajali za barabarani ili ziweze kuwalazimisha wamiliki wa vyombo hivyo kuimarisha huduma na kuwapunguzia kazi madereva kwa kuendesha mwendo mrefu kama hatua za kupunguza ajali za barabarani.

Maelekezo hayo yametolewa leo tarehe 03/06/2024 na Waziri wa Katiba na Sheria Dkt. Pindi Chana wakati akifungua kikao kazi cha Kamisheni ya Tume hiyo ambacho kimefanyika Mkoani Morogoro katika hoteli ya Morena kwa ajili ya kupitia taarifa saba (7) za utafiti uliofanywa hivi karibuni.

Waziri huyo ameeleza kwamba imekuwa ni utaratibu wa kawaida kwa wananchi kupoteza maisha na kupata ulemavu wa kudumu unaosababishwa na ajali za barabarani zinazotokana na makosa yanayoweza kuzuilika hasa kwa mabasi yaendayo masafa marefu.

“Umefika wakati Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania kufanya utafiti na kuja na mapendekezo madhubuti yatakayo saidia kuondoa ajali za barabarani ili kulinda afya na maisha ya watanzania kwa kuwalazimisha wamiliki kuajiri dereva zaidi ya mmoja katika chombo kimoja cha masafa marefu” alisema Waziri

Aidha ameagiza Tumehiyo kushirikiana na wasimamizi wa sheria ya barabaraniili kutafuta suluhisho la kudumu la kuwalinda wasafiri kwa usalama na kuhakikisha wanafika kwa wakati, huku akiligusia swala la bima za maisha katika kuwasidia wathirika.

“Sisi kama wabobevu wa sheria lazima tuangalie kama kampuni inapata ajali za mara kwa mara waachane na biashara ya kusafirisha watu na badala yake wasafirishe mizigo.” alisema

Aidha ameendelea kueleza kwamba Tume ya Kurekebisha sheria kupitia wizara ya katiba na sheria ambao ndio wenye dhamanahazipotayari kuona tayari kuona wananchi wakipoteza maisha kila kukicha.

Aidha, ameitaka Tume ya kurekebisha sheria wasisubiri kuletewa kazi za utafiti au mapitio kama ilivyo sasa na badala yake wafanye kulingana na wanavyoona hali halisi na wanayoyapata wakati wa utafiti.

**Bashiri S. Juma**

**Kitengo cha Mawasiliano Serikalini- LRCT**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**TUME YA KUREKEBISHA SHERIA TANZANIA**

***Chuo Kikuu cha Dodoma,Barabara ya Mkalama,Jengo la Taaluma Na.1,S.L.P. 1718, Dodoma.***
***Tovuti: www.lrct@lrct.go.tz; Barua pepe: lrct@lrct.go.tz; Simu: +255734 356685/****6*